Ecolebooks.com

# DARASA LA NANE

DIGITAL DITION
022

# SIGNAL EXAMS 2020

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA**
**KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.

9. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.
    **Mfano**
    **Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Chagua silabi sahili kati ya hizi.
   A. ng
   B. d
   C. wa
   D. chwa

Jibu sahihi ni C (**wa)**

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

**1** [A] [B] [C] [D]   **1** [A] [B] [C] [D]   **21** [A] [B] [C] [D]   **31** [A] [B] [C] [D]   **41** [A] [B] [C] [D]

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

SIGNAL

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

-

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa**

© *All rights reserved. No direct reprint, duplication, photocopying or sharing on social media platforms without the prior written permission of the publisher.*

**Signal Publishers Limited**

Signal Exams @Signalexams



ECOLEBOOKS.COM

***Soma vifungu vifuatavyo.Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Serikali ___1___ wananchi wote kutunza afya ___2___. Wananchi wenye afya ___3___ kutekeleza shughuli mbalimbali za kuindeleza nchi kiuchumi ___4___ watapunguzia serikali gharama ya kushughulikia matibabu. Hata hivyo, ___5___. Kufanikiwa kwa juhudi za serikali ___6___ kwa kiasi kikubwa jinsi wananchi wenyewe ___7___ kujitunza. Miongoni mwa ___8___ iliyowekwa ni bima ya afya inayohakikisha kuwa wananchi wanapata matibabu bila malipo.

**1.** A. ingekuwa iliwahimiza    B. inakuwa ikiwahimiza
C. imekuwa ikiwahimiza    D. ilikuwa ingewahimiza

**2.** A. zao    B. zenu    C. zake    D. yako

**3.** A. wanaweza tu    B. hawawezi tu    C. hawawezi kamwe    D. wakaweza kamwe

**4.** A. kwani pia    B. bali pia    C. mbali na    D. ilhali

**5.** A. hakuna mchele ukosao ndume    B. kitanda usichokilalia hujui kunguni wake
C. penye miti hapana wajenzi    D. ukibebwa usilevyelevye miguu

**6.** A. inategemea    B. zinategemea    C. kunategemea    D. watategemea

**7.** A. wanavyojitahidi    B. wanaojitahidi    C . wanayojitahidi    D. wanapojitahidi

**8.** A. hatua    B. mikakati    C. lengo    D. mambo

Ziara yetu katika eneo la Bonde la Ufa ___9___ sana. Tulijionea ___10___ ya kupendeza kama vile Kasoko ya Long'onot, Ziwa Naivasha na ndege wa ziwani waitwao ___11___. Walimu wetu ___12___ kwamba haya ni ___13___ muhimu sana kwa uchumi wetu. Huko Olkaria, ___14___ kuona umeme ukizalishwa kwa nguvu za mvuke ___15___ ardhini.

**9.** A. ilifaa    B. ilifana    C. ilifaana    D. ilifanana

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. mandari | B. mazingara | C. mandhari | D. maajabu |
| **11.** | A. chozi | B. nondo | C. bundi | D. heroe |
| **12.** | A. walitujuza | B. walitujulia | C. walijulisha | D. waliwajulisha |
| **13.** | A. rasilimali | B. malighafi | C. mazigazi | D. maliasili |
| **14.** | A. tunaajabia | B. tukiajabia | C. tuliajabia | D. tungeajabia |
| **15.** | A. zitokazo | B. itokayo | C. zitokapo | D. utokao |

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

**16.** Chagua sentensi yenye kiwakilishi cha nafsi ya tatu.
A. Wanaenda mashambani mwao.
B. Nilikipata kijiko pale.
C. Unataka nikusaidie vipi?
D. Tutaanza kusoma moja kwa moja.

**17.** Bainisha matumizi mwafaka ya ritifaa.
A. Kuonyesha kuwa kuna orodha inayofuata.
B. Kutambulisha sauti inayotamkiwa puani.
C. Kuonyesha sauti ambayo ni ghuna.
D. Kutambulisha maneno halisi yaliyotamkwa.

**18.** Ni orodha ipi iliyo na kasoro?
A. Nyigu, panzi, kumbikumbi.
B. Kizibao, kanzu, bwelasuti
C. Kitovu, shavu, kisigino.
D. Ujira, ubwete, pete.

**19. Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendwa.**
Mtoto alikula chakula akashiba.
A. Mtoto aliliwa chakula akashiba.
B. Chakula kililiwa mtoto akashiba.
C. Chakula kililiwa na mtoto akashiba.
D. Mtoto alilishwa chakula akashiba.

**20. Tambulisha kihusishi katika sentensi ifuatayo.**
Mtama wote ulianikwa nje ya nyumba ile.
A. ile B. nje ya
C. wote D. nyumba ile

**21.** Tamko lipi hutolewa na mtu anayetarajia kutamka maneno ambayo huenda yakaudhi hadhira yake?
A. Ashakum B. Simile
C. Samahani D. Pole

**22. Tumia kiulizi kifaacho zaidi.**
Musila aliumia mguu_____?
A. ipi B. mgani
C. mbona D. lini

**23.** Bainisha sentensi iliyo na **'kwa'** kuonyesha sababu.
A. Alitembea kwa madaha ya tausi.
B. Wazee kwa vijana walifika hapo.
C. Fundi alilipanda jengo kwa ngazi.
D. Ulikemewa kwa utovu wa nidhamu.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

**24. Kanusha sentensi ifuatayo.**
Mgeni akiondoka tutaanza shughuli nyingine.
A. Mgeni asipoondoka hatutaanza shughuli nyingine.
B. Mgeni akiondoka hatutaanza shughuli nyingine.
C. Mgeni asipoondoka tutaanza shughuli nyingine.
D. Mgeni hataondoka wala hatutaanza shughuli nyingine.

**25.** Mahali jikoni penye bomba la kuoshea vyombo ni
A. dohani B. karo
C. kichaga D. shubaka.

**26. Chagua jozi iliyo na methali zenye maana moja.**
*(i) Aliye kando haangukiwi na mti. (ii) Usipoziba ufa utajenga ukuta.*
*(iii) Cheche ya moto huchoma msitu. (iv) Tone na tone huwa mchirizi.*
A (ii) na (iii) B. (i) na (iv)
C. (iii) na (iv) D. (ii) na (iv)

**27.** Korija moja hujumulisha vitu vingapi?
A. Viwili B. Kumi na viwili
C. Ishirini D. Mia.

**28.** Chagua jibu sahihi.
A. Mjusi alituuzia mchuzi mtamu.
B. Doa yao haikuwa na doa hata kidogo.
C. Alikaanga kanga vizuri tukafurahia. D. Danda alidadia lori lilipopita hapa.

**29.** Shairi lenye mishororo miwili katika kila ubeti ni ______ ilhali shairi la majibizano huitwa _______.
A. tarbia, utenzi B. tathlitha, ngonjera
B. mizani, utenzi D. tathnia, ngonjera

**30.** Ni sentensi gani iliyo na kiigizi sahihi?
A. Aisee! Mambo usemayo ni ya kitoto.
B. Hewala! Hilo usemalo haliwezekani.
C. Oiyee! Tumefunga bao la ushindi.
D. Kefule! Nitakusaidia utakavyo.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

***Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali 31- 40.***

Ulemavu ni hali ya kuwa na kasoro katika viungo vya mwili. Upungufu huu huchangiwa na mambo mbalimbali. Pengine mtu anaweza kushindwa kutekeleza baadhi ya shughuli za kawaida kama vile kuongea, kutangamana na wengine, kusoma au hata kujitegemea kwa mambo mbalimbali. Mara nyingi ulemavu huwa wa kudumu japo kuna ule uwezao kuisha baada ya kipindi fulani.

Baadhi ya watu hupata ulemavu kutokana na kasoro wakati wa kufanyika kuwa mtoto tumboni. Huenda mzazi akajifungua salama lakini baadaye akagundua kuwa mtoto wake amekosa kiungo fulani. Pia, mtoto anaweza kuendelea kukua bila kugunduliwa lakini mabadiliko yanayotarajiwa katika vipindi mbalimbali vya ukuaji yakakosekana. Hata hivyo, wakati mwingine mabadiliko yanaweza kuchelewa lakini mwishowe yakatokea tu.

Mbali na hayo, binadamu anapotangamana na mazingira yake, anaweza kuambulia ulemavu kutokana na majeraha ya viungo, ya ubongo au uti wa mgongo. Magonjwa kama vile kisukari na shinikizo la damu pia yanaweza kuchangia ulemavu. Baadhi ya watu **waliokuwa wazima** hivi majuzi tu wameambulia ulemavu kupitia ajali mablimbali. Ni vyema mtu ajizatiti kuepuka hali yoyote inayoweza kuhatarisha afya yake.

Unaweza kufikiria kuhusu siku uliyoteleza mlipokuwa mkicheza na wenzako, ukateguka mguu au mkono? Pengine unakumbuka namna ulivyoteseka kwa kushindwa kujifanyia mambo muhimu kama vile kuoga, kutembea kuenda haja au hata kula. Yamkini utaniambia kuwa lililokuuma zaidi ya uchungu wa jeraha hilo  hilo ni kule kukosa fursa katika shughuli za kila siku. Hata wenzako walipokuzuru kukujulia hali, ulifurahi lakini ukavaliwa na ukiwa pindi tu walipokupa mgongo. Walemavu wengi hupitia hali kama hizi aushi yao yote.

Wakati mwingine watu huzitonesha nyoyo za ulemavu bila kujali hisia zao. Utamsikia mtu kwa mfano akisema, 'Niitie huyo **chongo** nimtume' au 'Msaidieni huyo kiwete jamani.' Sharti ieleweke kwamba walemavu ni binadamu wa kawaida na kila mtu anao ulemavu wa aina fulani. Hakuna aliye na wepesi wa kufanya kila kitu. Hata kuwa na **moyo wa harara** ni ulemavu mkubwa. Tukumbuke ya wahenga kuwa hucheka kovu asiyefikwa na jeraha. Watu hawa wana majina yao. Tusiwadhalilishe kwa kuwarejelea kwa maumbile yao.

Wapo wazazi wanaowaficha wana wao walemavu na hata kukosa kuwapeleka shuleni. Huu ni ukandamizaji wa hali ya juu. Mtu yeyote akipata nafasi ya kutangamana na mazingira yake ipasavyo, bila shaka atabuni njia ya kutekeleza shughuli zake kadri awezavyo.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON EC LEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

Walemavu wengine wameinukia kuwa watu wa kutegemewa sana na jamii, hata kiasi cha kuwafikia kuwafaa wale wasio na uatilifu wowote.

Kila binadamu ana haki zake. Ni vyema jamii ikubali kuwa waatilifu ni binadamu wanaohitaji huduma kama wengine wowote. Haki zao zitambuliwe na maumbile yasiwe kigezo cha kuwadhalilisha kwa vyovyote vile.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

**31.** Chagua maelezo sahihi kulingana na aya ya kwanza.
A. Ulemavu ni hali ya mtu kushindwa kufanya jambo.
B. Huenda mlemavu akashindwa kujihudumia ipasavyo.
C. Ulemavu wowote ule huwa ni hali ya kudumu.
D. Walemavu hushindwa kabisa kutekeleza shughuli muhimu maishani.

**32.** Kipi si kiini cha ulemavu?
A. Kuhusika katika ajali.
B. Kasoro za kimaumbile.
C. Mwili kukosa kuendelea ipasavyo.
D. Uchelewaji katika kukua.

**33.** **Waliokuwa wazima** kulingana na makala haya ni wale
A. ambao kasoro zao hazikuwa zimegunduliwa
B. ambao si watoto kwani wamekomaa
C. wasiokuwa na kasoro zozote za kimaumbile
D. waliofikiria kuwa hawawezi kuathirika.

**34.** Kulingana na aya ya nne
A. kuteleza kwa msimulizi kulimfanya mlemavu
B. mwandishi ana uhakika kuwa msomaji aliteleza michezoni
C. watoto waliopata majeraha hawaogi wala kutembea
D. kushindwa kujumuika na wengine huathiri hisia zaidi.

**35.** Ni hali gani ambazo mwandishi anasema walemavu wengi hupitia auishi yote?
A. Hali ya upweke na kunyimwa nafasi ya kushiriki.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

B. Ukiwa baada ya marafiki waliozuru kuaga haraka
C. Majeraha ya viungo na kulala siku nzima.
D. Kupuuzwa na marafiki na kuhitajika kutoa msaada.

**36.** Si vizuri kuwataja watu kulingana na kasoro zao kwani
A. huku ni kuwaumiza hisia zao
B. wana majina yanayojulikana na wote
C. huenda wasijue maana ya majina hayo
D. hata sisi ni walemavu kama wao.

**37.** ‘**<u>Chongo</u>**’ kulingana na makala haya ni
A. mtu ambaye mboni za macho yake zimeelekea kombo
B. mtu asiye na uwezo wa kuona kabisa
C. mtu ambaye jicho lake moja limepofuka
D. mtu mwenye nundu mgongoni pake.

**38.** Wazazi huwanyima watoto wao walemavu haki zipi?
A. Elimu na malezi.
B. Utangamano na makazi.
C. Mapenzi na makazi.
D. Shule na hiari.

**39.** Maana ya kuwa na ‘**<u>moyo wa harara</u>**’ ni
A. kushtuliwa na mambo madogo
B. hali ya kukasirika upesi
C. kutumia maneno makali kwa wengine
D. kuwa na maradhi ya moyo.

**40.** Kichwa kifaacho zaidi kwa makala haya ni
A. Haki za walemavu.
B. Vyanzo vya ulemavu.
C. Aina mbalimbali za ulemavu.
D. Ukarimu wa malemavu.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 – 50.***

Daktari Maluki alikaa katika chumba cha matibabu akijisikilizia muziki kwenye rukono yake. Alikuwa amefika kazini saa chache zilizopita. Akili zake zilikuwa mbali kidogo.Aliwaza kuhusu kima cha pesa na muda aliotumia kusomea taaluma hii. Akalinganisha na 'mshahara tonge' aliopata kama alivyouita yeye, japo mshahara wenyewe ulikuwa wa kuliliwa ngoa na akina yahe. Aliona kweli kwamba dunia haina huruma. Alipiga darubini na kuwaona jinsi viongozi wakuu walivyojilimbikizia donge nono licha ya kuwa walifanya kazi kwa muda mfupi sana.

Baada ya kutia na kutoa, aliibuka na uamuzi aliohisi kwamba ungemfaa bila 'kuwaathiri sana' waliosaka huduma yake. Kwanza, yetote aliyesaka huduma yake angelipa kifunguamkoba cha shilingi elfu mbili ili apate nafasi ya kumwona. Maadamu, alikuwa daktari mkuu, uamuzi wake haukupingwa sana pale hospitalini. Si kila mmoja anafahamu vyema kuwa mkono mtupu haurambwi? Tena yeye Daktari Maluki hakumwalika yeyote kuja kumwona. Si wanaletwa na shida zao tena kwa hiari yao?

Mradi huu ulifanikiwa sana na kumfurahisha Daktari Maluki. Sasa kipaji kilionekana kumnawiri wakati wote akiwa kazini. Aidha, aliiraukia kazi mapema sana ili aweze kuwahudumia wagonjwa wengi kadri ilivyowezekana. Kufanikiwa kwa mradi huu kulimfanya azuke na mwingine. Alifungua duka kubwa la dawa mkabala wa hospitali ile. Wagonjwa waliokuwa wakija kwa matibabu walikuwa wakipewa dawa dukani pale. Serikali ndiyo iliyolaumiwa kwa kukosa kuleta dawa hospitalini. Lakini sikwambii kuwa dawa zizo hizo zilizokuwa halali na haki yao ndizo walizozilipia pale dukani.

Daima dawamu ~~mbio za sakafuni huishia ukingoni. Siku moja, wasamari~~a wema walikuja na mgonjwa aliyehusika katika ajali ya barabarani. Alikuwa akivunja damu sana hivyo basi alihitaji kushughulikiwa kwa haraka. Daktari aliitwa lakini hakubanduka pale kitini mwake. Alitaka kujua ni nani angegharamia matibabu. Wasamaria wema hawakutaka kufanya hiyo maadamu **hawakuhusiana na mwele yule kwa damu wala usaha**. Basi mgonjwa akaachwa kuendelea kuvunja damu.

Watu waliokuwepo walishauriana na kuafikiana kuchanga angaa kifungua mkoba ili mgonjwa ahudumiwe. Hata zilipotosha walimwendea mgonjwa ili wampeleke kwa daktari. Lo! Walishangaa walipogundua kuwa mwili wake ulikuwa u baridi tayari. Daktari alitia fulusi kibindoni na kuagiza aletwe. Alipompimapima, aligundua kuwa amekata kamba. Hata

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

hivyo, alivutiwa na jingine. Ni uso wa mtu aliyemfahamu sana. 'Haiwezekani......mama........ mam....' Daktari akazirai.

Kumbe mamaye Maluki alikuwa amekuja kumzuru mwanawe mjini alipopigwa dafrau na gari kabla ya kufika kwa mwanawe. Sasa alikuwa kaenda jongomeo baada ya kunyimwa huduma na mwanawe aliyemzaa, akamlea na kumsomesha kwa shida. Ama kweli, kigumba ni kwa nguruwe, kwa binadamu ki uchungu.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

Ecolebooks.com

**41.** Kulingana na aya ya kwanza, Daktari Maluki
A. aliketi ofisini kusikiliza muziki kwenye redio
B. alizingatia sana muziki wa rukono yake
C. hakuwa amekaa sana baada ya kufika hospitalini
D. hakuwa na hamu ya kuwahudumia wagonjwa.

**42.** Kwa nini Daktari Maluki alijipata akiwaza?
A. Alihisi kuwa malipo yake hayakulingana na hadhi yake kikazi.
B. Alitumia pesa na muda mrefu kusoma kuliko wenzake.
C. Mshahara wake ulikuwa ukililiwa ngoa na kina yakhe.
D. Alitaka kuwa kiongozi wa serikali apate donge nono.

**43.** Kulingana na aya ya pili
A. waliotafuta msaada kwa daktari hawakuathirika kwa uamuzi wake
B. nafasi ya Daktari kazini iliufanya uamuzi wake kufuatwa bila swali
C. mtu akiwa na shida hafai kupewa hiari ya kuwa na usemi wowote
D. mtu akitaka msaada bila kutoa chochote hafai kuhudumiwa popote.

**44.** Kunawiri kwa kipaji cha Daktari Maluki ni ishara kuwa
A. watu sasa wameanza kuja kwake kwa hiari yao
B. kuongezewa mshahara kazini kumempa raha aliyotamani
C. huduma anayotoa kwa wateja ni bora kuliko awali
D. shughuli ya kifisadi aliyoanza inampa kipato alichotamani.

**45.** Si kweli kusema kuwa
A. Daktari alipofika kazini mapema aliwajali wagonjwa
B. Daktari alianzisha biashara karibu na hospitali aliyofanyia kazi
C. watu walilipia ada kwa sababu ya kukosa hiari
D. wagonjwa walipata baadhi ya dawa pale hospitalini.

DOWNLOAD MORE RESOURCES LIKE THIS ON ECOLEBOOKS.COM

**46.** Chagua sifa za Daktari Maluki kulingana na makala haya.
A. Mzingatifu na mkatili.
B. Fisadi, asiye na utu.
C. Katili na mwenye bidii kazini.
D. Mlafi na anayetafuta kutambuliwa.

**47.** Kwa nini Daktari hakubanduka kitini alipoitiwa mgonjwa?
A. Alikuwa amezama mawazoni.
B. Hakujua kuwa mgonjwa alikuwa hatarini.
C. Hakuwa na hamu ya kazi siku ile.
D. Mgonjwa hakuwa amelipiwa ada iliyohitajika.

**48.** **'Hawakuhusiana na mwele yule kwa damu wala usaha'** ina maana kuwa
A. wasamaria wema hawakujuana na mgonjwa yule
B. daktari hakutaka kujihusisha na majeruhi yule
C. wasaidizi hawakuwa wa nasaba ya majeruhi yule
D. wasamaria wema hawakuwa na uhusiano na Daktari.

**49.** Kilichochangia kifo cha majeruhi ni
A. kutelekezwa
B. kukosa kufungua mkoba
C. kuchelewa kufika hospitalini
D. kupewa matibabu yasiyofaa.

**50.** Aya ya mwisho imetufahamisha kuwa
A. mtu anapoadhibiwa kwa makosa yake hafai kuhurumiwa
B. mtu akitendewa dhuluma atendeazo wengine hawazii matendo yake
C. mtu anapotendewa uovu uo huo aliozoea huona uchungu sana
D. Mtu anaweza kufurahi anapowadhulumu wengine lakini adhulumiwapo hivyo huona uchungu.